# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA AFYA

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA

# NYARAKA YA MKATABA WA KOTESHENI
**Kutumia njia ya "Force Account"**

**KWAAJILI YA**

## UTOAJI WA HUDUMA YA UFUNDI UJENZI WA NYUMBA YA MAKAZI YA MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA – (KWANGWA)

**Kotesheni Na:**
**ME/016/2021-22/MRRH/NS/16 Lot 1**

**Mwajiri:**
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara
S.L.P 21,
Musoma- Mara

**Mtoa Huduma (Fundi):**
Michael V. Kiondo
S.L.P 733,
Musoma- Mara

## Vifupisho

**GCC** General Conditions of Contract - *Masharti ya Jumla ya Mkataba - MJM*

**ICB** International Competitive Bidding -*Ushindani Zabuni Kimataifa -UZM*

**IFQ** Invitation for Quotation - *Mwaliko wa Kotesheni (Zabuni Ndogondogo) .- MK*

**NCB** National Competitive Bidding - *Zabuni Zinazoshindanishwa Kitaifa -ZZK*

**PE** Procuring Entity - *Taasisi Nunuzi - TN*

**PPA 2011** Public Procurement Act No. 7 of 2011 - *Sheria ya Ununuzi Katika Sekta ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 - PPA, 2011*

**SCC** Special Conditions of Contract - *Masharti Maalumu ya Mkataba -MMM*

**SP** Service Provider - *Mtoa Huduma - MH*

**SoR** Statement of Requirement - *Maelezo ya Mahitaji -MM*

**SIFQ** Standard Invitation for Quotation - *Mwaliko Sanifu wa Kotesheni - MSK*

**TIN** Tax Identification Number - *Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi- NUMK*

**VAT** Value Added Tax _ *Kodi ya Ongezeko la Thamani - KOT*

**YALIYOMO**

Sehemu


Vifupisho ........................................ 1

Makubaliano ya Mkataba ........................................ II

Barua ya Kukubali Kotesheni ........................................ III

Maelezo ya Mahitaji, Viwango na Vipimo Kiufundi ........................................ IV

Masharti ya Jumla ya Mkataba ........................................ V

Masharti Maalumu ya Mkataba ........................................ VI

Michoro ........................................ VII

Viambatisho ........................................ VIII

# SEHEMU IV: BARUA YA KUKUBALI KOTESHENI

# MAKUBALIANO YA MKATABA

Makubaliano haya ya Mkataba yanafanywa leo tarehe 19/04/2022 Kati ya HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA, S.L.P 21, MUSOMA (Hapa ataitwa "Mteja") kwa upande mmoja na 1. MICHAEL V. KIONDO, S.L.P 733 MUSOMA (Hapa ataitwa "Mtoa Huduma") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Mteja amekaribisha Kotesheni kwa kutoa huduma yaani: Ufundi ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara na amekubali Kotesheni ya Mtoa Huduma kwa huduma kwa jumla ya shilingi za Kitanzania Milioni Kumi Na Tatu Laki Tisatisini Na Sita Elf Mia Nne **(13,996,400.00) ikiwa malipo yaliyojumuisha Kiodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kwa Mkataba Na. ME/016/2021-2022/MRRH/NS/16 Lot 1** Hapa itaitwa ("Bei ya Mkataba").

**SASA MAKUBALIANO HAYA YAMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

1. Katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaolejelewa.

2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kutafasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani;

   i) Fomu ya Makubaliano ya Mkataba;
   ii) Barua ya Kukubali Kotesheni;
   iii) Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni;
   iv) Masharti Maalumu ya Mkataba;
   v) Masharti ya Jumla ya Mkataba;
   vi) Jedwali la maelezo ya kazi na mchanganuo wa Bei; (Schedule of labour).
   viii) Michoro (drawings)
   ix) Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba kama vile Barua za wadhamini watatu zinazokiri kumdhamini fundi husika.

3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo baadaye kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.

4 Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mteja kwa **Mtoa Huduma** kama baadaye inavyotajwa, **Mtoa Huduma** hapa anakubaliana na Mteja kutekeleza na kukamilisha Huduma kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote zile na kulingana na vifungu vya mkataba.

Mteja hapa anakubali kumlipa Mtoa Huduma kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa Ufundi ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, kwa jumla ya shilingi za Kitanzania Milioni Kumi Na Tatu Laki Tisa tisini na Sita Elf Mia Nne **(13,996,400.00)** ikiwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani **(VAT), kwa Mkataba Na. ME/016/2021-2022/MRRH/NS/16 Lot 1** baadaye imerejelewa kama "Bei ya Mkataba" kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

KATIKA KUSHUHUDIA, pande hizi zimefanya makubaliano ya kutekelezwa kulingana na sheria katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**IMETIWA SAHIHI KWA AJILI YA**
**NA KWA NIABA YA MWAJIRI (MTEJA)**

..................................................

**Sahihi**

(Jina): Omari R. Pyerr

(Wadhifa): Mganga Mfawidhi

..................................................

**Sahihi**

(Jina): Ridhiwani Saidi

MEDICAL OFFICER INCHARGE
MUSOMA REGIONAL REFERAL
HOSPITAL - MARA
P.O. BOX 21, MUSOMA

**KWA NIABA YA MTOA HUDUMA (FUNDI)**

..................................................

**Sahihi**

(Jina): MICHAEL V. KIONDO

(Wadhifa): MHANDISI

(Anwani): 733 MUSOMA

..................................................

**Sahihi**

(Jina): AMOS K. BILTON

(Wadhifa): FUNDI

(Anwani): 245 MUSOMA

# SEHEMU YA III : MAKUBALIANO YA MKATABA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**MKOA WA MARA**
Simu Na: 028-2620780
E-mail: musomarrh@afya.go.tz

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
Mkoa wa Mara,
S.L.P 21,
Musoma,
TANZANIA.

Kumb.Na: CDC.240/425/01A/25

12 Aprili, 2022

Michael V Kiondo
S.I.P 733
**MUSOMA**

## YAH : BARUA YA KUKUBALI KOTESHENI

1. Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu

2. Hii ni kukutaarifu kuwa kotesheni yako ya tarehe ***23/03/2022*** ya kutoa **Huduma ya Ufundi Ujenzi wa Nyumba ya Mganga Mafawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara** kwa bei ya Mkataba ya **Shilingi Milioni Kumi na Tatu Laki tisa Tisini na sita elfu Mia nne (13,996,400.00) ikiwa na kodi ya Ongezeko la Thamani**, kama ilivyosahihishwa na kurekebishwa ipasavyo na maelekezo kwa Mtoa Huduma sasa imekubaliwa.

3. Unatakiwa kuweka sahihi Makubaliano ya Mkataba na kuanza kutoa huduma katika ndani ya wiki moja tangu mkataba utakapotiwa sahihi.

4. Nakutakia Utekelezaji mwema

Dkt. Osimund Dyegura
**MGANGA MFAWIDHI**

MEDICAL OFFICER INCHARGE
MUSOMA REGIONAL REFERRAL
HOSPITAL - MARA

# SEHEMU V: MAELEZO YA MAHITAJI, VIWANGO NA VIPIMO KIUFUNDI

# SEHEMU VI: MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA

## A: VIFUNGU YA JUMLA

### Kifungu 1: Nyaraka za Mkataba

Masharti ya Mkataba na fomu ya Malezo ya mahitaji, Viwango na Vipimo ni sehemu muhimu ya nyaraka za Mkataba na zinapaswa kusomwa pamoja na nyaraka nyingine zote zinazounda Mkataba. Kama ikitokea kuna mgogoro, kipaumbele cha nyaraka kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Kifungu cha 6** cha Masharti haya ya Mkataba.

### Kifungu 2: Tafsiri

Katika Masharti haya ya Mkataba maneno yafuatayo yatakuwa na maana zilizotolewa kwayo kama ilivyo hapa chini:

| | |
|---|---|
| **Mteja** | Taasisi ya Serikali inayonunua huduma kama zilivyotajwa kwenye mkataba. |
| **Mtoa Huduma** | Mtu au watu au kampuni ambayo kotesheni yao imekubaliwa na mteja. |
| **Huduma** | Huduma itakayotolewa kulingana na mkataba. |

### Kifungu 3: Maelekezo

Maelekezo yanayotolewa na Mteja yatakuwa kwa maandishi. Kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yakatolewa kwa mdomo, Mtoa Huduma atafuata maelekezo hayo. Katika kipindi cha **siku 7** maelekezo yaliyotolewa kwa mdomo yanapaswa kuwa yamethibitishwa kwa maandishi.

### Kifungu 4: Lugha

Matangazo yote, maelekezo na mawasiliano au waraka wowote wa maandishi unaohusu mkataba utaelezwa bayana katika Masharti Maalumu ya Mkataba.

**Kifungu 5: Sheria inayotumika**

Mkataba, maana yake, fasiri yake, na utekelezaji wake vitaongozwa na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu 6: Nyaraka za Mkataba zenye Kipaumbele**

Nyaraka kadhaa zinazofanya mkataba zichukuliwe kuwa zinajieleza kikamilifu lakini kama ikitokea hitilafu yoyote ile nyaraka zenye umuhimu wa kwanza zitakuwa zifuatazo:

i) Fomu ya Makubaliano;
ii) Barua ya Kukubali Kotesheni;
iii) Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni & barua ya maombi;
iv) Masharti Maalumu ya Mkataba;
v) Masharti ya Jumla ya Mkataba;
vi) Michoro
vii) Maelezo ya Mahitaji na Orodha ya Bei (Schedule of labours); na
viii) Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba huu (Kumbukumbu za ufafanuzi, Muhtasari wa majadiliano, Barua za udhamini na nyaraka zinginezo muhimu).

**B: MAJUKUMU**

**Kifungu 7: Utekelezaji wa Mkataba**

**Mtoa Huduma (fundi)** atatoa nguvu kazi yote, zana za ufundi, usafiri /malazi kwa vibarua wake, maunzi na chochote kile kinachohitajika katika utoaji wa huduma **Mtoa huduma (fundi)** atatoa huduma kulingana na inavyotakiwa na nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakavyotolewa mara kwa mara na kama jinsi ilivyofafanuliwa kwenye masharti maalumu.

**Kifungu 8: Kutoa kazi kwa Mtoa Huduma Mwingine**

**Mtoa Huduma (Fundi)** hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Mtoa Huduma Mwingine bila kibali cha maandishi cha kutoka kwa Mteja. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei **Mtoa huduma(Fundi)** mamlaka au majukumu yake chini ya mkataba na **Mtoa huduma (Fundi)** atakuwa na wajibu kwa kushindwa au kuzembea kwa yeyote kati ya watoa huduma wake wasaidizi.

**Clause 9: Usimamizi wa Kazi wa Mtoa Huduma**

**Mtoa Huduma(Fundi)** atatoa huduma kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mteja ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, wingi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mteja anaona uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo kutoka katika kaida zilizowekwa, hatua zinazofaa zitachukuliwa na **Mtoa Huduma(Fundi)** ili kurekebisha hali. Mtoa huduma atawajibika kusogeza vifaa vya ujenzi kama ilivyofafanuliwa kwenye masharti maalumu ya mkataba.

**Kifungu 10: Ukaguzi**

Mteja au mwakilishi wake aliyempa mamlaka ana haki ya kukagua huduma na **Mtoa Huduma (fundi)** atatoa ushirikiano unaofaa wakati Mteja atakapohitaji kufanya hiyo.

**Kifungu 11: Huduma Zilizokataliwa**

Huduma zisizofuata mahitaji ya mkataba zitakataliwa. Kwa maelekezo ya Mteja, Mtoa huduma kwa gharama zake mwenyewe atarekebisha au kutoa upya huduma itakayokuwa imekataliwa hadi kumridhisha Mteja kikamilifu.

**Kifungu 12: Bima (Usalama wa Wafanyakazi na Vifaa.**

**Mtoa Huduma** ataweka bima yenye jina lake na la Mwajiri kwa ajili ya hasara au uharibifu wa zana, mitambo na maunzi, wizi na hali nyingine zinazolingana na hizo kwenye Ofisi ya Mwajiri, ambayo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa wafanyakazi wa Mtoa huduma. Mtoa huduma pia atatoa bima kwa ufidiaji majeruhi binafsi au kifo cha mfanyakazi wa **Mtoa Huduma (Fundi)** awapo kazini. (Mtoa huduma (fundi) atawajibika kwa usalama wa wafanyakazi wake na vifaa wakati wa utekelezaji wa kazi kwenye eneo la kazi.

**Kifungu 13: Wajibu wa Mtoa Huduma**

**Mtoa Huduma(Fundi)** atamkinga Mwajiri dhidi ya hasara au uharibifu wa upande wa tatu. Atamkinga kikamilifu Mwajiri wake dhidi ya madeni na hasara zinazotokana na Sheria ya Ajira na Fidia ya Wafanyakazi.

**Kifungu 14: Jambo Lisilozuilika**

Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambao pande zote za mkataba kwa hali ya kawaida zisingeweza kutabiri mapema, hasara au uharibifu kama huo utagharimiwa na **Mwajiri** na **Mtoa Huduma (Fundi)** kama vile Mafuriko, Vita, Kimbunga, Mabadiliko ya Sheria, Maelekezo ya Serikali na Majanga ya Moto na Mafuriko n.k

**Kifungu 15: Ubora wa Huduma na Usanifu wa Kazi**

Huduma zote na usanifu wa kazi vitakuwa vya aina na ubora kama ilivyofafanuliwa katika Mkataba na kulingana na maelekezo ya Mteja na vitaingizwa katika vipimo kama Mteja atakavyotaka.

**Kifungu 16: Upatikanaji wa Maunzi**

**Mtoa Huduma(Fundi)** atabainisha vyanzo vyote vya maunzi yanayohitajika kabla ya kuanza kutoa huduma. Mwajiri atalazimika kama itahitajika upatikanaji wa vyanzo vya maunzi hayo. **Mtoa Huduma (Fundi)** hatatumia maunzi yaliyobainiwa bila kuwa na kibali cha maandishi toka kwa Mwajiri.

**Kifungu 17: Kuondoka Eneo la Kutolea Huduma**

Baada ya kumaliza kutoa huduma, Mtoa huduma ataondoa zana zote, maunzi ya ziada na uchafu katika eneo la kutolea huduma na kuacha eneo hilo likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mwajiri.

**Kifungu 18: Afya, Usalama na Kulinda Mazingira.**

**Mtoa huduma(Fundi)** katika kipindi chote cha mkataba atazingatia kikamilifu masuala ya kiafya na kiusalama katika kanda yake ya kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari yoyote kwa watu hao.

**Mtoa Huduma (Fundi)** atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelezwa na Serikali ya Tanzania.

**Kifungu 19: Kuanza na Kukamilika Utoaji Huduma.**

**Mtoa Huduma(Fundi)** ataanza na kukamilisha huduma katika muda uliyoelezwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mteja.

**Kifungu 20: Ubadilishaji**

Mteja anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha huduma na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza **Mtoa Huduma(Fundi)** ipasavyo. Ubadilishaji huo utakuwa kwa Agizo la Mabadiliko ya Mkataba. Mteja ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na kima cha kizio kwenye Kotesheni au kama hakuna kima cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mteja na kukubaliwa na **Mtoa Huduma(Fundi).**

## C: MALIPO

**Kifungu 21:**

**21.1 Malipo wakati Kazi inaendelea**

Malipo yatafanywa kwa **Mtoa Huduma(Fundi)** wakati kazi inaendelea kila mwezi baada ya kuwasilisha ankara kama huduma iliyotolewa inalingana na masharti ya mkataba.kuanzia Kwa kila ankara kiasi cha fedha kilichotajwa kwenye Masharti Maalum ya Mkataba kitashikiliwa lakini hakitazidi asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Fedha anayotakiwa kulipwa **Mtoa Huduma(Fundi)** chini ya Ankara yoyote ile italipwa na Mwajiri kwenda kwa Mtoa Huduma katika kipindi kitakachokuwa kimetajwa katika Masharti Maalumu ya Mkataba baada ya Ankara kuwasilishwa na **Mtoa huduma(Fundi)**

**21.3 Makato ya Malipo**

Mteja atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi cho chote, fedha ya malipo ya awali au madeni yanayolipika kutoka kwa **Mtoa**

**Huduma(Fundi)** kwenda kwa Mteja kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa **Mtoa Huduma(Fundi)** na Mteja chini ya mkataba huu ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria pengine ambayo mteja anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

**21.4 Malipo kwa Wafanyakazi**

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi/vibarua na /au malipo ya kukodisha zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mteja atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya **Mtoa Huduma(Fundi).** Mteja atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa **Mtoa Huduma(Fundi)** mishahara yao na fidia nyingine na madeni ya kukodisha vifaa. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na **Mtoa Huduma (Fundi)** kutoka kwa Mteja chini ya mkataba huu.

**Kifungu 22: Malipo ya Ucheleweshaji Huduma**

Kama Mtoa Huduma(Fundi) atashindwa kutoa huduma katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wowote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, **Mtoa Huduma(Fundi)** atamlipa Mteja malipo ya ucheleweshaji katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku hadi kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba.

## D: KUSULUHISHA MIGOGORO NA KUVUNJA MKATABA

**Kifungu 23: Kusuluhisha Migogoro**

23.1 Kama migogoro ikitokea itasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote. Kama baada ya siku thelathini (30) pande hizo zimeshindwa kumaliza mgogoro au tofauti zao kwa majadiliano ya pamoja, upande wowote ule utawasilisha mgogoro huo kwa maandishi kwa Mwamuzi na kutoa nakala kwa upande mwingine.

23.2 Mwamuzi aliyetajwa katika **Masharti Maalumu ya Makataba** atatoa maamuzi kwa maandishi katika muda wa siku ishirini na nane (28) baada ya kupokea taarifa ya mgogoro.

23.3 Mwamuzi atalipwa kwa saa kwa kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** pamoja na kurudishiwa gharama za aina ya matumizi kama yalivyobainishwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** na gharama hiyo itagawanywa kati ya Mteja na **Mtoa Huduma(Fundi)** kwa uamuzi wowote utakaofikiwa na Mwamuzi. Upande wowote unaweza kupeleka uamuzi wa Mwamuzi kwa Msuluhishi kwa maandishi katika kipindi cha siku ishirini na nane (28) baada ya uamuzi ya Mwamuzi. Kama hakuna upande wowote utakaokuwa umepeleka mgogoro kwa Msuluhishi katika muda wa siku ishirini na nane (28) zilizotajwa hapo juu, uamuzi wa Mwamuzi utakuwa ndiyo wa mwisho na itabidi ufuatwe.

23.4 Kama Mwamuzi atajiuzulu au kufariki au kama Mteja na **Mtoa Huduma(Fundi)** wakikubaliana kuwa Mwamuzi hafanyi kazi yake ipasavyo kulingana na vifungu vya Mkataba, Mwamuzi mpya atateuliwa kwa pamoja kati ya Mteja na **Mtoa Huduma(Fundi).** Kama kuna kutokubaliana kati ya Mwajiri na **Mtoa Huduma** katika muda wa siku 30, Mwamuzi atateuliwa na Mamlaka ya kuteua itakayotajwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** kwa maombi ya upande wowote katika muda wa siku kumi na nne (14) tangu kupokelewa kwa ombi hilo.

23.5 Mgogoro au tofauti yoyote ambapo notisi ya kusudio la kuanza usuluhishi imetolewa kulingana na kifungu hiki itamalizwa kwa usuluhishi. Usuluhishi unaweza kuanza kabla au baada ya kuanza kutoa huduma chini ya mkataba.

23.6 Usuluhishi utaendeshwa kulingana na taratibu za usuluhishi kama zilivyochapishwa na taasisi iliyotajwa na mahali palipoonyeshwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba.**

23.7 Bila kujali uwepo kwa usuluhishi wa aina yoyote,

(a) Pande zote zitaendelea kutekeleza majukumu yao chini ya mkataba isipokuwa kama wakikubaliana vinginevyo; na

(b) Mwajiri atamlipa Mtoa Huduma fedha yoyote Mtoa Huduma anayodai.

**Kifungu 24: Uvunjaji wa Mkataba**

24.1 Kama **Mtoa Huduma(Fundi)** anashindwa kuanza kutoa huduma katika muda uliopangwa au kuna sababu za kutosha kuamini kuwa hatakamilisha huduma katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe ya kukamilisha au anashindwa kufuata moja ya masharti au hafuati maelekezo ya Mteja au anakuwa mufilisi, Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri **Mtoa Huduma(Fundi)** mpya wa kutoa huduma hiyo.

24.2 Kama Mteja atashindwa kumlipa **Mtoa Huduma (Fundi)**katika muda wa siku 60 baada ya tarehe ya kuwasilisha madai, Mtoa Huduma atakuwa na haki ya kuvunja mkataba.

**Kifungu 25: Malipo kama Mkataba Umevunjwa**

Kama Mkataba umevunjwa, **Mtoa Huduma(Fundi)** atalipwa na Mteja fedha au maunzi yatakayokuwa bado hayajalipiwa katika malipo atakayokuwa amelipwa **Mtoa Huduma(Fundi)** kwa huduma zote zitakazokuwa zimetolewa kabla ya kuvunja mkataba kwa kima na bei kama ilivyotolewa kwenye Mkataba. Ilimradi tu wakati wote itakuwa dhidi ya malipo yoyote yaliyo tayari kutoka kwa Mteja chini ya kifungu hiki, Mwajiri atakuwa na haki ya kulipwa fedha yoyote toka kwa **Mtoa Huduma(Fundi)** iliyotokana na malipo ya awali, kutokana na mitambo/zana/magari na maunzi, na kiasi cho chote alicholipwa **Mtoa Huduma(Fundi)** na Mteja kwa ajili ya utoaji wa huduma.

# SEHEMU VII: MASHARTI MAALUMU YA MKATABA

Taarifa maalumu ifuatayo kwa ajili ya Huduma Zisizo za Ushauri wa Kitaalamu zinazonunuliwa na itakuwa nyongeza, au inaweza kurekebisha vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba**. Kunapokuwa na mgogoro, vifungu katika Masharti Maalumu ya Mkataba vitakuwa na nguvu zaidi ya vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba.**

| Masharti Maalumu ya Mkataba Kifungu Na. | Masharti ya Jumla ya Mkataba Kifungu Na. | Marekebisho ya, na Nyongeza kwa vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba |
|---|---|---|
| 1 | *2.0* | Namba ya mkataba: **NA. ME/016/202122/MRRH/NS/16 / Lot 1**<br>Meja ni **: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara**<br><br>Eneo la utekelezaji **ni :** Eneo la Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwal J.K Nyerere - **Kwangwa**<br><br>Msimamizi wa Mradi ni**: Mhandisi kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mara**<br><br>Huduma: **ufundi ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mganga mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara (Kwangwa).** |
| 2 | 4.0 | Lugha ya Mkataba: *Ni Kiswahili, kwa maelekezo yaliyo katika lugha ya kiingereza yatatolewa tafsiri na Mhandisi wa Ujenzi (M) kabla na wakati wa utekelezaji wa mkataba.* |
| 3 | 7.0 | Fundi atapaswa kuleta mpango kazi wake wa kila wiki na anapaswa kuzingatia utekelezaji wake. |
| 4 | 7.1 | Fundi (mtoa huduma) atapaswa kuleta majina ya fundi Mwashi na fundi chuma. |
| 5 | 8.0 | Fundi(mtoa huduma) hapaswi kubadilisha mafundi wasaidizi bila idhini ya Msimamizi wa mradi. |
| 6 | 9.0 | Mtoa huduma (fundi) atapaswa kusogeza vifaa vya ujenzi kutoka kwenye eneo la kazi lenye ukubwa wa ekari 2 kama jinsi lilivyoainishwa kwenye mchoro yaani "site plan" kwa idhini ya Msimamizi wa mradi na kuviweka kwenye jengo analojenga ili kuendelea na kazi. |
| 7 | 18.0 | Fundi (mtoa huduma ) haruhusiwi kushawishi wenzake kuungana kwa lengo la kuhujumu mradi (vitendo vyote |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuungana kwa lengo la kuhujumu mradi (vitendo vyote vinavyoweza kusababisha mradi usiendelee).Ikithibitika amefanya hivyo mkataba wake utasitishwa mara moja. |
| 8 | 19.0 | Utekelejazi wa Mkataba Unaanza ndani ya wiki moja (1) baada ya siku ya kutia sahihi mkataba. |
| 9 | 19.0 | Muda wa kukamilisha kazi ni ndani ya miezi mitatu (3) baada ya siku ya kutia sahihi mkataba |
| | 21.0 | Malipo yatafanyika kwa mujibu wa bei ya mkataba iliyotajwa kwenye fomu ya makubaliano, Fundi atapaswa kukamilisha ujenzi wa jengo kwa gharama (bei) hiyo iliyotajwa kwenye fomu ya makubaliano ambayo ni kiasi cha shilingi za Kitanzania hakutakuwa na malipo ya ziada isipokuwa kwa idhini ya Msimamizi wa mradi akiona kuna umuhimu wa kufanya hivyo baada ya kupata Kibali kwa Mganga Mfawidhi. |
| 10 | 21.1 | Malipo ya awali (kama yatalipwa) ni ***Hakuna malipo ya awali. ya bei ya Mkataba (N/A)***<br><br>Nyongeza inayokubalika itakuwa katika aina ya dhamana ya Benki makataa (irrevocable) kutoka benki inayoaminika kwa kiasi kinachofanana. |
| 11 | 21.2 | Asilimia ya fedha za kushikiliwa: **[*Kipengele hiki hakihusiki (N/A)*]** ya thamani ya madai kwa mwezi huo.<br><br>Fedha iliyoshikiliwa itatolewa katika [*ingiza kipindi*] baada ya kukamilika kwa mkataba.**(Kipengele hiki hakihusiki)**<br><br>Kiasi anachopaswa kulipwa **Mtoa Huduma (Fundi)** chini ya Ankara yoyote kitalipwa na Mteja kwa **Mtoa Huduma (Fundi)** baada ya fundi kutekeleza kazi kwa kiwango kulingana na Kipengele husika kwenye **Schedule of Labour** baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa mradi (Mhandisi wa Ujenzi na pia baada ya kukaguliwa na kuridhiwa na Timu ya Usimamizi wa Ujenzi. |
| 12 | 21.4 | Kama Mteja atashindwa kufanya malipo katika [*Ingiza Kipindi*] Mteja atamlipa **Mtoa Huduma** riba katika kima [*Ingiza kima cha riba*]**Kipengele Hiki hakihusiki(N/A)** |
| 13 | 23.2 | Mwamuzi (Msuluhishi) atakuwa ***Mahakama ya Tanzania*** |

| | | |
|---|---|---|
| | | Aina ya gharama zitakazorudishwa zitakuwa ***Gharama za kujikimu*** |
| **15** | **23.4** | Mamlaka ya kuteua Mwamuzi ni **Wakala wa majengo (TBA) Mkoa** |
| **16** | **23.6** | Taasisi ya Usuluhishi itakuwa ***Mahakama ya Tanzania***<br><br>Mahali pa kufanyia Usuluhishi Ni ***Ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.*** |

## SEHEMU VIII

## JEDWALI LA MAELEZO YA KAZI NA MCHANGANUO WA BEI (SCHEDULE OF LABOUR)

# SCHEDULE OF LABOUR'S

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - Shs |
|---|---|---|
| A | **Msingi wa Jengo (Sub-structure)** | |
| 1 | Kuseti jengo | 382,500/= |
| 2 | Uchimbaji wa msingi | 648,700/= |
| 3 | Kufukia | 105,000/= |
| | **Kufunga mbao** | |
| 4 | Pembezoni mwa jamvi | 293,000/= |
| 5 | Pembezoni mwa nguzo | 293,000/= |
| 6 | Kuondoa mbao | 105,000/= |
| | **Kumwaga zege** | |
| 7 | Chini kwenye msingi wa tofali | 208,000/= |
| 8 | Chini kwenye msingi wa nguzo | 208,000/= |
| 9 | katika nguzo ya awali | 208,000/= |
| 10 | kwenye jamvi | 308,000/= |
| 11 | Ujenzi wa tofali (994 No) | 769,750/= |
| | **Mawe** | |
| 12 | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | 386,500/= |
| 13 | Umwagiliaji wa maji | 70,000/= |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | 3,985,000/= |
| B. | **Kunyanyua jengo (Super-structure)** | |
| 1 | Ujenzi wa tofali za kuta na uwekaji DPC (1759No) | 1,785,000/= |
| | **Kufunga mbao katika:** | |
| 2 | Nguzo mlalo | 293,250/= |
| 3 | Nguzo wima | 293,250/= |
| | **Kusuka nondo katika:** | |
| 4 | Nguzo mlalo | 386,500/= |
| 5 | Nguzo wima | 386,500/= |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| 6 | Nguzo mlalo | 308,000/= |
| 7 | Nguzo wima | 308,000/= |
| 8 | Umwagiliaji wa maji | 70,000/= |
| C. | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | |
| | Kuezeka na ufungaji wa gata | 1,500,000/= |
| | **Jumla ndogo kunyanyua jengo** | 5,330,500/= |

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - Shs |
|---|---|---|
| D. | **Milango** | |
| 1 | Kufitisha fremu za milango | 398,475/= |
| 2 | Kufitisha shata za milango pamoja na vitasa | 398,475/= |
| 3 | Upakaji wa Varnishi katika milango na fremu | 201,250/= |
| | | |
| E. | **Umaliziaji (Finishing)** | |
| | *Upigaji wa lipu pamoja na kutengeneza koplo:* | |
| 1 | Nje ya jengo | 800,000/= |
| 2 | Ndani ya jengo | 800,000/= |
| | | |
| | **Sakafu** | |
| 3 | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) | 500,000/= |
| 4 | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) - | 600,000/= |
| | | |
| | **Dali:** | |
| 6 | Ufungaji wa mbao za dali (Brandering) | 300,000/= |
| 7 | Uwekaji wa dali na mikanda ya gypsum | 400,000/= |
| 8 | Uwekaji wa dali ya pvc kuzunguka nyumba kwa nje | 250,000/= |
| | | |
| 9 | Uwekaji wa vigae katika kuta na upakaji grout | 280,000/= |
| | **Jumla ndogo umaliziaji(finishing)** | 5,328,200/= |
| | | |
| | | |
| F. | **Rangi na Mapambo (Painting & Decoration)** | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu pamoja na skimming katika:** | |
| 1 | Kuta za nje | 400,000/= |
| 2 | Kuta za ndani | 550,000/= |
| 3 | Dali | 150,000/= |
| | | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu katika:** | |
| 5 | Msingi wa nyumba | 100,000/= |
| 6 | Grill za milango na madirisha | 200,000/= |
| | | |
| | **Jumla ndogo Rangi na mapambo** | 1,400,000/= |
| | | |
| G. | **Umeme (Electrical installation)** | |
| 1 | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | 400,000/= |
| 2 | Usukaji wa umeme awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 400,000/= |
| | **Jumla ndogo Umeme** | 800,000/= |

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - Shs |
|---|---|---|
| H. | **Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)** | |
| | | |
| 1 | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | 400,000/= |
| 2 | Ufungaji bomba awamu ya pili (2nd fix) -fittings | 250,000/= |
| 3 | Ufungaji wa Mifumo ya maji ya mvua kwenda kwenye tanki | 100,000/= |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na taka** | 750,000/= |

| | MAJUMUISHO (SUMMARY) | Shs |
|---|---|---|
| A. | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | ~~3,985,000/=~~ 3,985,5 (6/04) |
| B. | Kunyanyua jengo (Super-structure) | 3,830,500/= ✓ |
| C. | Kuezeka (Roof structure and covering) | 1,500,000/= ✓ |
| D. | Milango | 998,200/= ✓ |
| E. | Umaliziaji (Finishing) | ~~4,330,000/=~~ 4,030,0 (6/) |
| F. | Rangi na Mapambo (Painting & Decoration) | 1,400,000/= ✓ |
| G. | Umeme (Electrical installation) | 800,000/= ✓ |
| H. | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | 750,000/= ✓ |
| | **JUMLA KUU Shs.** | ~~17,593,700/=~~ |

17,294,200/=.

06/04/202

**ANGALIZO**:


Fundi anatakiwa kujaza hii fomu kwa kupitia mchoro wa jengo husika

SEHEMU VII :
MAELEKEZO YA UFUNDI (SPECIFICATION)
YAMEAMBATISHWA.

## SEHEMU VII: MICHORO

(*Ingiza MICHORO kama ipo*)

| DOOR & WINDOW SCHEDULE | | | |
|---|---|---|---|
| NO. | WIDTH | HEIGHT | TOTAL |
| D1 | 900mm | 2500mm | 8 |
| D2 | 800mm | 2100mm | 3 |
| W1 | 1500mm | 1500mm | 9 |
| W2 | 600mm | 600mm | 3 |




# GROUND PLAN

SCALE: 1:100

TOTAL AREA = 93sqm

Building Sector
Policy and Planning Department
Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children
University of Dodoma
College of Humanities and Social Sciences
Building,
P. O. Box 743,
40478 DODOMA

Approved


| No. | Description | Date |
|---|---|---|
| | | |

Client
PRESIDENT OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Project
PROPOSED HEALTH CENTER

**STAFF QUARTERS**
**Ground Floor Plan**

| | | |
|---|---|---|
| Project number | 2018 / 02 / 01 | A I O I |
| Date | 02 FEBRUARY 2018 | |
| Drawn by | DCNM | |
| Checked by | DCNM | Scale 1: 100 |





# ROOF PLAN
SCALE: 1:100

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Building Sector<br>Policy and Planning Department<br>Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children<br>University of Dodoma<br>College of Humanities and Social Science Building<br>P. O. Box 743,<br>40478 DODOMA | Approved | No. | Description | Date | Client<br>PRESIDENT OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATIONN AND LOCAL GOVERNMENT<br>Project<br>PROPOSED HEALTH CENTER |

**STAFF QUARTERS**
**Roof Plan**


| | | |
|---|---|---|
| Project number | 2018 / 02 / 01 | A102 |
| Date | 02 FEBRUARY 2018 | |
| Drawn by | DCNM | |
| Checked by | DCNM | Scale 1: 100 |





# SECTION X:X
SCALE: 1:50

| Building Section<br>Policy and Planning Department<br>Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children<br>University of Dodoma<br>College of Humanities and Social Science ... Building,<br>P. O. Box 743,<br>40478 DODOMA | Approved | No. | Description | Date | Client<br>PRESIDENT OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT<br>Project<br>PROPOSED HEALTH CENTER | STAFF QUARTERS<br>Section X:X |
|---|---|---|---|---|---|---|


| | | |
|---|---|---|
| Project number | 2018 / 02 / 01 | A I 03 |
| Date | 02 FEBRUARY 2018 | |
| Drawn by | DCNM | |
| Checked by | DCNM | Scale 1:50 |





FRONT ELEVATION




RIGHT SIDE ELEVATION




REAR ELEVATION





LEFT SIDE ELEVATION

# ELEVATIONS
SCALE: 1:100

| Bahi Sector Policy and Planning Department Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children University of Dodoma College of Humanities and Social Science ... Bahi, P. O. Box 743, 40478 DODOMA | Approved | No. / Description / Date | Client: PRESIDENT OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT<br>Project: PROPOSED HEALTH CENTER | STAFF QUARTERS<br>Elevations |
|---|---|---|---|---|

| No. | Description | Date |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| Project name | 2018 / 02 / 01 | A104 |
| Date | 02 FEBRUARY 2018 | |
| Drawn by | DCNM | |
| Checked by | DCNM | Scale 1:100 |




FOUNDATION PLAN

**NOTE:**

1. All dimensions are in mm unless otherwise specified
2. All discrepancies shall be referred to the structural engineer
3. Reinforced concrete shall be of grade 20 with fcu=25N/mm² at 28 days of age
4. Main reinforcements shall be high tensile steel with fy = 460N/mm²
5. Nominal cover to the reinforcements:
   a) Foundation 50mm
   b) Column 25mm
   c) Beam 25mm
   d) Slab 25mm


PROJECT:
**PROPOSED REHABILITATION OF HEALTH CENTRE**

CLIENT: **PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATI[illegible] LOCAL GOVERNMENT**


**MINISTRY OF HEALTH, COMMUNITY DEVELOPMENT GENDER AND CHILDREN**

DRAWING TITLE:
**STAFF HOUSE FOUNDATION LAYOUT**


| | |
|---|---|
| Designed by: | Eng. R.A.M |
| Drawn by: | ENG. MKHOTYA |
| Checked by: | Eng. R.A.M |
| Approved by: | |
| Date: 2018 | Scale: |
| Drawing No. STR.101 | Sheet: |





Section B - B




Section C - C




COLUMN FOOTING F1 -Nos
1000x1000x250mm




TYPICAL SECTION A-A THROUGH FOOTING

# FOUNDATION DETAILS

**NOTE:**

1. All dimensions are in mm unless otherwise specified
2. All discrepancies shall be referred to the structural engineer
3. Reinforced concrete shall be of grade 25 with fcu=25N/mm² at 28 days of age
4. Main reinforcements shall be high tensile steel with fy = 460N/mm²
5. Nominal cover to the reinforcements:
   a) Foundation 50mm
   b) Column 25mm
   c) Beam 25mm
   d) Slab 25mm

PROJECT:

**PROPOSED REHABILITATION OF HEALTH CENTRE**

CLIENT:


**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION LOCAL GOVERNMENT**

**MINISTRY OF HEALTH,COMMUNITY DEVELOPMENT,GENDER, ELDERLY AND CHILDREN**

DRAWING TITLE:

**STAFF HOUSE PLINTH BEAM LAYOUT**

| | |
|---|---|
| Designed by: | Eng. R.A.M |
| Drawn by: | Eng. R.A.M |
| Checked by: | ENG. A.MKHOTYA |
| Approved by: | |
| Date: 2018 | Scale: |
| Drawing No. STR,102 | Sheet: |




# FOUNDATION BEAM LAYOUT

**NOTE:**

1. All dimensions are in mm unless otherwise specified
2. All discrepancies shall be referred to the structural engineer
3. Reinforced concrete shall be of grade 25 with fcu=25N/mm² at 28 days of age
4. Main reinforcements shall be high tensile steel with fy = 460N/mm²
5. Nominal cover to the reinforcements:
   a) Foundation 50mm
   b) Column 25mm
   c) Beam 25mm
   d) Slab 25mm

PROJECT:

**PROPOSED REHABILITATION OF HEALTH CENTRES**


CLIENT:

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATIO LOCAL GOVERNMENT**


**MINISTRY OF HEALTH,COMMUNITY DEVELOPMENT,GENDER, ELDERLY AND CHILDREN**

DRAWING TITLE:
**STAFF HOUSE PLINTH BEAM LAYOUT**


| | |
|---|---|
| Designed by: | Eng. R.A.M |
| Drawn by: | Eng. R.A.M |
| Checked by: | Eng. A. MKHOTY/ |
| Approved by: | |
| Date: **2018** | Scale: |
| Drawing No. **STR,103** | Sheet: |





BEAM 01 230x300mm




BEAM 07 230x300mm




SECTION A-A




SECTION B-B

**NOTE:**

1. All dimensions are in mm unless otherwise specified
2. All discrepancies shall be referred to the structural engineer
3. Reinforced concrete shall be of grade 25 with fcu=25N/mm² at 28 days of age
4. Main reinforcements shall be high tensile steel with fy = 460N/mm²
5. Nominal cover to the reinforcements:
   a) Foundation 50mm
   b) Column 25mm
   c) Beam 25mm
   d) Slab 25mm

PROJECT:

**PROPOSED REHABILITATION OF HEALTH CENTRES**

CLIENT:

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION LOCAL GOVERNMENT**

**MINISTRY OF HEALTH,COMMUNITY DEVELOPMENT,GENDER, ELDERLY AND CHILDREN**

DRAWING TITLE:

**STAFF HOUSE PLINTH BEAM DETAILS**

| | |
|---|---|
| Designed by: | Eng. R.A.M |
| Drawn by: | Eng. R.A.M |
| Checked by: | Eng. A.MKOTYA |
| Approved by: | |
| Date: **2018** | Scale: |
| Drawing No. **STR.104** | Sheet: |

## SEHEMU VIII: FOMU MBALIMBALI

*[Ingiza nembo, Anwani Kamili ya Posta, na simu, fasimili na namba ya teleksi na anwani ya Barua pepe]*

# REKODI YA MAJADILIANO

Jina la Taasisi Nunuzi: HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA (KWANGWA

Kotesheni Na.: ME/016/2021-22/MRRH/NS/16 Lot 1 & Lot 2

Maada ya Manuunzi: UTOAJI WA HUDUMA YA UFUNDI UJENZI WA NYUMBA YA MAKAZI YA MGANGA MFAWIDHI NA NYUMBA YA MAKAZI YA MTUMISHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA - (KWANGWA)

Aina ya Ununuzi: Huduma zisizo za kitaalam

Tarehe ya Majadiliano: 12/04/2022

| SEHEMU 1: REKODI YA MAJADILIANO | |
|---|---|
| **MAADA** | **MAKUBALIANO (TAARIFA KAMILI)** |
| 1. Majadiliano ya bei ya Mkataba | Kupunguza gharama za ufundi ujenzi kutoka Tshs 17,294,200.00 hadi Tshs 14,000,000.00. Mzabuni aliafiki kufanya majadiliano ya kupunguza bei ya awali ili kufikia lengo la bajeti ya hospitali. Mwisho wa majadiliano kiasi kilichoafikiwa na wajumbe na mzabuni ni Tshs 13,996,400.00. |
| 2. Vipengele vilivosahaulika<br>a. Kusuka nondo za ulalo na za wima za kwenye Msingi<br>b. Mfumo wa maji taka (Septic and Soak away pit)<br>c. Kitako cha tanki ya kuvuna maji ya mvua | Wajumbe walibaini kusahaulika kwa vipengele vitatu muhimu ambavyo vinaathiri gharama za ujenzi.<br>Hata hivyo kipengele cha kwanza (kusuka nondo za wima na za mlalo kwenye msingi) mzabuni aliafiki gharama hiyo iingizwe kwani iko ndani ya uwezo wake na haitaathiri gharama ya mwisho ya bei baada ya majadiliano.<br><br>Wajumbe walishauri vipengele viwili vilivyobaki vifanyiwe kazi ya thamini yaani mchoro na gharama za ufundi kabla ya mzabuni kusaini mkataba. |

Tunathibitisha yaliyoandikwa hapo juu ni rekodi ya kweli na sahihi ya majadiliano yaliyofanyika.

| ~~Ununuzi na Ugavi~~ - Dkt. KWA NIABA YA TASISI NUNUZI | Mzabuni |
|---|---|
| Sahihi: [signature] | Sahihi: [signature] |
| Jina: Dr Mary R. Mahenge | Jina: MICHAEL KIONDO |
| Cheo: MO | Cheo: MHANDISI |
| Tarehe: 12/04/2022 | Tarehe: 12/04/2022 |

**Kiambatanisho:**
Muhtasari wa kikao cha majadiliano.

# OMBI LA IDHINI YA MPANGO WA MAJADILIANO .

*(Iidhinishwe na Bodi ya Zabuni)*

Jina la Taasisi Ununuzi: HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA-KWANGWA Kotesheni Na.: ME/016/2021-22/MRRH/NS/16 Lot 1 & Lot 2

Maada ya Manuunzi: UTOAJI WA HUDUMA YA UFUNDI UJENZI WA NYUMBA YA MAKAZI YA MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA MARA – (KWANGWA)

Aina ya Ununuzi: Huduma zisizo za kitaalam

Timu ya Majadiliano kwa mujibu wa kanuni 226(6) ya GN Na 446 ya mwaka 2013 imeandaa mpango wa majadiliano .

| Na. | Eneo la Majadiliano | Lengo | Vigezo vya Majadiliano |
|---|---|---|---|
| 01. | Gharama za Mkataba | Kupunguza gharama za ufundi ujenzi kutoka Tshs 17,294,200.00 hadi Tshs 14,000,000.00 | Kukubaliana na Mzabuni kupunguza gharama za ufundi ujenzi kutoka Tshs 17,294,200.00 hadi Tshs 14,000,000.00 |
| 02. | Muda wa utekelezaji wa Mkataba | Muda wa utekelezaji wa mkataba unatakiwa uwe ndani ya miezi mitatu tangu kusainiwa kwa mkataba. | Kukubaliana na mzabinu/fundi muda wa mkataba uwe ndani ya miezi mitatu tangu kusainiwa kwa mkataba. |

Nawasilisha Mpango wa Majadiliano kwa ajili ya kuuidhinisha.

| Mwenyekiti wa Timu ya Majadiliano |
|---|
| Sahihi: [signature] |
| Jina: Dr Mary Malunge |
| Tarehe: 12/04/2022 |

Mpango wa Majadiliano umekubalika/haujakubalika kwa mujibu wa kanuni 227 (1) ya GN Na. 446 ya mwaka 2013.

| Katibu wa Bodi ya Manunuzi | Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni |
|---|---|
| Sahihi: [signature] | Sahihi: [signature] |
| Jina: Nicodemus Shemzigwa | Jina: DR Elias Gwadiny |
| Tarehe: 12/04/2022 | Tarehe: 13/04/2022 |

**MICHAEL VICTOR KIONDO,**
**S.L.P 733,**
**MUSOMA.**
**0713854001**
michaelkiondo65@gmail.com.

**02/04/2022**

**MGANGA MFAWIDHI,**
**HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MARA,**
**S.L.P 21,**
**MUSOMA.**

**YAH: MAOMBI YA FUNDI MSIMAMIZI WA KAZI ZA UJENZI (Local fundi)**

Mimi Mhandisi Michael Victor Kiondo, naomba kutoa huduma ya ufundi ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya mtumishi wa Hospital ya Rufaa Mkoa wa Mara – (Kwangwa) yenye Kotesheni Na: **ME/016/2021-22/MRRH/NS/16 Lot 1.**

Utekelezaji wa kazi hii itagharimu Milioni kumi na saba laki tano tisini na tatu elfu mia saba **(Tshs. 17,593,700/=)** itachukua muda wa **Miezi miwili na nusu.**

Naamini maombi yangu yatashughulikiwa ipasavyo na kupewa kipa umbele mkubwa.

Wako Katika Utekelezaji

……………………………………

**Mhandisi**
**Michael Victor Kiondo**

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.



KATA YA KITAJI
04/04/2022

OFISI YA MTENDAJI
KATA YA KITAJI
S.L.P 194,
MUSOMA.
4/04/2022.

MGANGA MFAWIDHI,
HOSPITARI YA RUFAA,
YA MKOA WA MARA,
S.L.P 21.
MUSOMA.

YAH: UTAMBULISHO WA NDUGU MICHAEL VICT KIONDO.

Rejea mada tajwa hapo juu

Ofisi yangu Inamtambulisha Kwako mtajwa hapo juu ni mkazi hala wa Kata ya Kitaji mtaa wa Kitaji B nyumba namba 33 Manispaa ya musoma mkoa wa Mara.


Ni matumaini yangu Kuwa OFISI yako itampa uduma yoyote ataka yo itaji

Wako Katika Utumishi wa Uma

A.Byabachwezi
ARAN BYABACHWEZI.
AFISA MTENDAJI
KATA YA KITAJI
04/04/2022

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

OFISI YA MTENDAJI WA KATA
KATA YA KAMUNYONGE
S·L·P 194, SIMU 0752869568
MUSOMA




KMB·AMK/UT/KMG/12 04/04/2022

MGANGA MFAWIDHI(M)
S·L·P 21
MUSOMA

YAH: UTAMBULISHO WA NDUGU MAGIRA LAZARO MAGIRA.

Nathibitisha kwamba mtajwa hapo juu ni mtanzania harisi, mkazi halali katika eneo langu la utawala mtaa wa majita road, barabara ya mzalendo.

Ofisi yangu haina shaka juu ya mwenendo wake na uhami nifu wake katika jamii. Shughuli zake ni ukandarasi wa majengo na barabara.

Nashauli apokelewe na Akubaliwe kupata huduma/kazi katika taasisi yako ya umma.

Wako katika utumishi wa umma

MATHIAS·M·MAKUNJA

MTENDAJI WA
KAMUNYONG

MAGIRA LAZARD MAG
S.L.P 888,
MUSOMA.
0767249490

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA
MKOA WA MARA
S.L.P. 21
MUSOMA

YAH: UDHAMINI WA NDUGU MICHAEL KIONDO

Mada tajwa hapo juu yahusika, mimi Magira Lazaro Magira mkazi wa kamnyonge, namdhamini ndugu Michael Kiondo kwa kazi aliyoomba ya ujenzi wa Nyumba ya Mganga Mfawidhi na mtumishi

Natanguliza shukrani zangu za dhati kwako katika ujenzi wa Taifa

Magira L. Magira

[signature]

HALIMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.




OFISI YA MTENDAJI
KATA YA KITAJI
S.L.P 194,
MUSOMA.
4/04/2022

MGANGA MFAWIDHI
HOSIPITARI YA RUFAA
MKOA WA MARA
S.L.P 24
MUSOMA.

YAH; UTAMBULISHO WA NDUGU DOGO ISRAEL MGOB. AMBAE NI MDHAMINI WA NDUGU MICHAEL VI KIONDO.

Rejea mada tajwa hapojuu.

Ofisi yangu inapenda kumtambulisha kwako ndugu mtajwa hapojuu ku wa ni mkazi wa kataya kitaji mtaa wa kitaji B nyumba namba barabara ya mkendo, ambae ni mdhamini wa ndugu Michael Victor Kiondo.

Ni matumaini yangu kuwa watapata huduma stahiki kutoka ofisi yako.

Wako katika utumishi wa uma.

A. Byabachwezi
ARAN BYABACHWEZI
Afisa mtendaji Kitaji

KATA YA KITAJI

DOGO I MUGOBI
P.O BOX 194
MUSOMA
0768437199
4/3/2022

MGANGA MFAWIDHI
HOSIPITALI YA RUFAA
MKOA WA MARA
P.O BOX 21
MUSOMA.

YAH KUMDHAMINI NDUGU MICHAEL VICT

Rejea Kichwa cha habari hapo juu
Mimi DOGO I MUGOBI nakubali kumdhamini ndugu michael Victor Kiondo kwenye huduma ya ujenzi wa nyumba ya makazi ya mganga mfawidhi wa mkoa wa mara katika eneo la kwangwa natanguliza shukurani za dhati kwako kwa kumwamini kumpatia huduma hiyo na nitatoa ushirikiano wa dhati pindi nitakapohitajika

Wako katika ujenzi wa taifa
Dogo I MUGOBI

Domi

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.



AFISA MTENDAJI
KATA YA KITAJI
04/04/2022

OFISI YA MTENDA
KATA YA KITAJ
S.L.P 194.
MUSOMA.
04/04/2022.

MGANGA MFAWIDHI,
HOSIPITARI YA RUFAA,
MKOA WA MARA,
S.L.P 21,
MUSOMA.

YAH: UTAMBULISHO WA NDUGU ROSE WILLI OMOLO AMBAE NI MUDHAMINI WA NDUG MICHAEL VICTOR KIONDO.

Rejea mada tajwa hapojuu.

Ofisi yangu inapenda kumtambulisha kwako ndugu Rose willison Omolo kuwa ni mkazi wa Kata ya Kitaji mtaa wa Kitaji B nyumba namba barabara ya Welfare, ambae ni mdhamini wa Michael Victor Kiondo.

Nimatumaini yangu watapewa huduma wanayo itaka kutoka kwe ofisi yako.

Mtumishi katika utumishi wa umma

Abyabalwazi
ARAN BYABALWEZ
Afisa mtendaji Kata ...

AFISA MTENDAJI
KATA YA KITAJI
04/04/2022

ROSE WILSON OMOLLO
P.O. BOX 733
0769 900994
MUSOMA
2/4/2022

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITAL YA RUFAA
MKOA WA MARA
P.O. BOX 21
MUSOMA

YAH: KUMDHAMINI NDUGU MICHAEL VICTOR KIONDO KWENYE HUDUMA YA UJENZI

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Mimi Rose Wilson Omollo nakubali kumdhamini Ndugu Michael Victor Kiondo kwenye huduma ya Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi wa hospitali katika Mkoa wa Mara katika eneo la Kwangwa. Natanguliza shukrani za dhati kwako kwa kumwamini kumpatia huduma hiyo na nitatoa ushirikiano wa dhati pindi nitakapohitajika.

Wako katika Ujenzi wa Taifa
Rose Wilson Omollo

RWilson.